

Kupalilia Kuondoa Kwekwe

Mashamba ya mikundi yanafaa kuondolewa kwekwe ili:

- Kupunguza kuwepo kwa maradhi ya aina mbalimbali kama vile *woodiness* na virusi vya cucumbea *mosaic*.
- Kupunguza makao ya kuzaliana ya nematodi na pia kupunguza ile hali ya kwekwe kutumia rutuba inayohitajika na mikundi.

Unyunyizaji

Milimita 1,200 za mvua kwa mwaka zinatoshia lakini ni vyema kunyunyizia ikiwa mvua ni haba.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Kahinga, J.N

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI-Thika S.L.P. 220 Thika, 0100

Simu: (067) 212281/5, 21134

Simu ya kusambaza: 2055038

Nukulishi: (067) 21285

Baruapepe: karithika@africaonline.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 10 /2008

Shilingi 20 za Kenya

**Namna ya kutayarisha
kishamba cha matunda
aina ya karakara (passion)**



Utangulizi

Shamba la matunda ya karakara lililotayarishwa vyema kutoka mwanzoni huwa na mimea yenye nguvu na afya ambayo hustahimili janga za kimazingira kwa jumla.



Mchanga

Mchanga ni lazima ufanyiwe utafiti wa kutambulisha aina yake, udani wake, viwango vya kemikali, viwango vya maadili na viwango vya nematodi.

Mchanga ufaayo zaidi ni ule mwepesi hadi mzito aina ya mseto unaoshikana. Kiasi cha kemikali (ph) cha 5.5 hadi 6.5 kinahitajika.

Utayarishaji ardhi

Hufanywa miezi 2 hadi 3 kabla ya kupanda. Sehemu gumu zilizo sentimita 80 zivunjiwe.

Kupanda

Mashimo yenye upana wa sentimita 45 (1.5 feet) na undani wa sentimita 45, nafasi ya 1.8 katika mishororo. (katikati ya mimea) na mita 2 katikati ya mishororo.

Mbolea

Mikundi hupendezwa sana na mbolea. Tia angalau kilo 10 za mbolea iliyokomaa vyema na uchanganye vizuri na mchanga.

Fosiforasi

Unafaa kutia gramu 125 za *Triple super Phosphate (TSP)* au *Diammonium Phosphate (DAP)* kwa kila shimo. (Aina utakayotumia italingana na kiwango cha kemikali (ph) ya mchanga.

Nitrojeni

Calcium Ammonium Nitrate (CAN) hutwiwa wiki mbili baada ya kupanda kiasi cha gramu 120 kwa kila mmea. Inaweza kutiwa kama imegawanywa.

Vifaa vya kuegemea

Mikundi hutambaa na kwa hivyo huhitaji vifaa vya kuegemea.

- Mashimo yenye undani wa sentimeta 50 huchimbwa yakiwa na nafasi ya mita 6 katikati mwa mishororo ya kupandia.
- Vikingi vitakayotumiwa vunafaa kuwa na mita 2.7.



Kuchumia matawi

Kuchumia kunahitajika lakini kwa kiwango cha chini na hufanywe kunapohitajika tu.

- Kuchumia matawi huchangia kukua upya na urahisisha katika kuzuia maradhi na wadundu.
- Huwezesha kung'olewa kwa sehemu za mimea nyonge na zilizokufa.